



## Ndoa za Mapema na za Kulazimishwa

**Kumlazimisha mtu yeyote kuolewa ni uhalifu mbaya nchini Australia.**

Nchini Australia, watu wako huru kuchagua kama wanataka kuoa au kuolewa. Kwa kawaida, mtu lazima awe na zaidi ya umri wa miaka **18** ili kuolewa kisheria. Katika baadhi ya mazingira mtu mwenye umri wa zaidi ya miaka 16 anaweza kuolewa, lakini hii inahitaji amri ya mahakama.

Mtu lazima akubaliane na ndoa bila kulazimishwa au kudanganywa.

Ndoa za kukubaliana, ambapo watu wawili kwa uhuru wao wanakubali kuoana, ni tofauti na ndoa za kulazimishwa. Ndoa za kukubaliana zinakubalika kisheria nchini Australia.

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko hatarini, wapigie simu polisi, nambari ya simu **000**.  
Polisi nchini Australia ni wazuri na wanaweza kuaminiwa.

Kwa maelezo na ushauri wa faragha bila malipo, piga simu 1800 RESPECT nambari ya simu **1800 737 732**.

Kama unahitaji mkalimani bila malipo piga simu **131 450**.

**Ni kinyume cha sheria kuchukua au kutuma mtu kwenda nchi nyingine kufanya ndoa za kulazimishwa au kutumia mtu mwingine kupanga hii.**

Ndoa ya mapema na kulazimishwa wakati mwingine inahusishwa na kuwahamisha watu kwenda nchi nyingine au kuvuka mipaka kinyume na matakwa yao, na hii ni kinyume cha sheria.

**Je wewe, au mtu mwingine unayemjua, yuko hatarini?**

Pigia simu **Australian Federal Police (Polisi Wakuu wa Australia)** (AFP) nambari ya simu **131 237**. AFP inaweza kutoa ushauri wa mapema na kuwaelekeza waathiriwa wa ndoa za mapema na za kulazimishwa au biashara haramu ya binadamu waweze kupata msaada, ikiwa ni pamoja na malazi, msaada wa kifedha, ushauri na ushauri wa kisheria.

Kwa maelezo zaidi fuata kiungo kwenye tovuti ya AFP [www.afp.gov.au](http://www.afp.gov.au).

**Kuna huduma nyingi nchini Australia ambazo zinaweza kukusaidia.**

**1800 RESPECT** ni Australia's National Sexual Assault, Family and Domestic Violence Counselling service (Huduma ya Ushauri wa Mzozo wa Kijinsia, Uhasama wa Kifamilia na Kinyumbani kutoka kwa Taifa la Australia) . Hutoa simu bila malipo na ushauri na maelezo mtandaoni. Washauri watakusikiliza, watajibu maswali na kukuelekeza kwa huduma nyingine za usaidizi katika eneo lakoi.

Pigia simu **1800 737 732** au nenda kwenye tovuti ya 1800 RESPECT [www.1800RESPECT.org.au](http://www.1800RESPECT.org.au)

**Je unahitaji mkalimani?**

Pigia **Translating and Interpreting Service (Huduma ya Utafsiri na Ukalimani)** (TIS) bila malipo, nambari ya simu **131 450**. TIS inaweza kukusaidia kuwasiliana na huduma nyingine. TIS haitoi ushauri.

**Kwa maelezo zaidi kuhusu ndoa za kulazimishwa na biashara haramu ya binadamu:**

Fuata kiungo kilicho kwenye tovuti ya Attorney-General's Department (Idara ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali) iliyo [www.ag.gov.au](http://www.ag.gov.au).